



OFISI YA WAZIRI MKUU SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI

www.pmo.go.tz

DODOMA TOLEO LA OCTOBA 2022



Katibu Mkuu
Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu
2 Barabara ya Posta 40412 Dodoma Tanzania



www.pmo.go.tz



Vikao vya Mashirikiano kuendelea kufanyika

Serikali imedhamiria kuendeleza kufanya Vikao vya Mashirikiano ili kufanya tafakari ya pamoja juu ya shughuli zinazofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais Zanzibar.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene katika mkutano wa kwanza wa Vikao vya Mashirikiano katika ngazi ya Mawaziri kilichofanyika Ukumbi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Kikwajuni Zanzibar.

“Kushirikiana huku hakuepukiki na kwa bahati nzuri serikali zote ni za Chama Cha Mapinduzi lazima tukutane mara kwa mara ili tuweze kutathimini ni namna gani tunatekeza ilani ya Uchaguzi”.

Hii ni hatua nzuri tumefikia na ni lazima tuboreshe ratiba zaidi, ili tuende zaidi ya kiwango tunachokwenda sasa, alisema Waziri.

“Tusiishie kukutana ngazi hii tuu, tuweke utaratibu wa uratibu wa kukutanisha makundi na hasa vijana ili waweze kuufahamu Muungano wetu na wauenzi ili uwe na faida iliyokusudiwa na waasisi wetu wa Nchi hizi Mbili”.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi Mhe. Hamza Hassan Juma amesema Muungano wetu ni wa kipekee na kuendelea kukutana hivi ni kuimarisha mawazo ya waasisi wetu wa Muungano.

“Tunakaa tunazungumza mambo ya Wizara na taasisi zetu lakini tunakumbushana umuhimu wa Muungano na umoja wetu”.



RAIS SAMIA MGENI RASMI UZINDUZI MATOKEO YA SENA YA WATU NA MAKAZI

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi Uzinduzi wa Matokeo ya Mwanzo ya Sena ya Watu na Makazi, Sena ya Majengo na Sena ya Anwani za Makazi ya Mwaka 2022 pamoja na muongozo wa matumizi ya matokeo hayo.

Uzinduzi huo utakaofanyika katika uwanja wa Michezo wa Jamhuri hapa jijini Dodoma ambao takwimu zake ndio zitatumika katika kupanga matumizi mbalimbali nchini, wakiwemo wabunge ambao watautumia muongozo huo kujua changamoto za majimbo na kuzitatua.

Hayo yamesemwa jijini hapa leo, Oktoba 28, 2022 na Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu George Simbachawene wakati akizungumza na Waandishi wa habari huku akiwataka wananchi mkoani hapa kujitokeza kwa wingi kushuhudia tukio hilo 31 Oktoba, 2022.

“Oktoba 31 ni siku maalum kwa taifa letu hivyo basi hatuna budi kuhakikisha kwa tuliopo Dodoma na mikoa ya jirani tunajitokeza kwa wingi uwanja wa Jamhuri na wale tutakaokuwa mbali tufuatilie uzinduzi huo kupitia vyombo vya habari ili tushiriki pamoja na Mheshimiwa Rais kujua tupo wangapi wakati atakapotangaza Matokeo hayo ya Mwanzo,” amesema

Amesema kuwa uzinduzi huo ni tukio muhimu katika historia ya maendeleo ya nchi ndio maana Serikali imeamua kuhakikisha kunakuwa na uwakilishi wa wananchi wa makundi yote ili waweze kushiriki katika tukio hili la kihistoria.

“Sensa ya Watu na Makazi hufanyika mara moja kila baada ya miaka kumi na matokeo yake ndio yanayotumika katika kufanya maamuzi yote muhimu yanayohusu maendeleo ya nchi kwa kipindi cha miaka kumi hadi Sensa nyingine, hivyo Sherehe hizi za uzinduzi wa Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 zitahudhuriwa na viongozi wote wakuu wa Serikali pamoja na Marais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Marais wastaafu wa Zanzibar,” amesema

Amesongeza kuwa katika uzinduzi huo pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na Marais hao wastaafu watatunukiwa tuzo maalum kwa kufanikisha Sensa katika vipindi vya uongozi.

Simbachawene amewataja Waalikwa wengine kuwa ni viongozi wa Serikali wakiwemo mawaziri na manaibu waziri, Makatibu wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu wa Serikali zetu zote mbili, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, viongozi wa vyama vya Siasa na wawakilishi wa makundi mbalimbali katika jamii.

“Wageni wengine mashuhuri ni pamoja na Waheshimiwa Mabalizi wanaowakilisha nchi zao humu nchini, Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa yakiwemo ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika na Wadau wengine



“WAZIRI SIMBACHAWENE, WEKEZENI DODOMA”

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati hiyo Dkt. Joseph Mhagama aliipongeza Serikali ya Awamu wa Sita kwa namna inavyowezesha ujenzi wa Mji wa Serikali kwenda kwa kasi na hii inafaa kuungwa mkono.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Mhe Dkt. Joseph Mhagama akizungumza mara baada ya kujionea na kujiridhisha

“Ninampongeza Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kuendeleza Mji huu, na Kamati imeridhishwa na maendeleo ya ujenzi hivyo ninawapongeza ofisi ya Waziri Mkuu kwa kufanya kazi kwa weledi,” alisema Dkt. Mhagama

Akitoa neno mjumbe wa kamati hiyo Mhe. Asha Abdallah ametoa kongole kwa kazi kubwa inayofanywa na serikali huku akiwaasa watanzania kutumia mji huo katika kupata huduma kwakuwa unafikika kwa wepesi.

“Ofisi hizi kupatikana mahali pamoja ni jambo nyeti litakalopunguza kero kubwa za wananchi kwani wizara zote zitafikika kwa wepesi, jueni kuwa serikali haijawatupa inajali sana,”

Naye Mjumbe wa Kamati hiyo Mhe. Salum Shafi amesema kila mmoja aone umuhimu wa kulinda na kutunza majengo yatakayotumika na kuhakikisha wanakuwa wazalendo.

“Mradi huu ni fedha za walipa kodi, hivyo kila mmoja awe mzalendo katika kutunza na kulinda yaweze kutumika kwa muda mrefu katika ubora wake na kuongeza tija katika shughuli za Serikali ,hakika Dodoma imepambika na mama ameifanya kazi vizuri mama tunakupongeza,” alisisitiza



Waziri Simbachawene awapa kongole timu za michezo Ofisi ya Waziri Mkuu

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera mbio za baiskeli na riadha.

Bunge na Uratibu) Mhe: George Waziri alitumia fursa hiyo kuwaasa Simbachawene amezipongeza timu za wanamichezo wa ofisi hiyo kuongeza kasi michezo za ofisi ya Waziri Mkuu kwa kwenye kushiriki michezo licha ya kushiriki na kupata ushindi wakati wa michezo kuwa ni ajira kwa wanamichezo mashindano ya michezo ya Shirikisho la wengine lakini pia inaleta afya na kujenga Michezo ya Wizara na Idara za Serikali mahusino mazuri baina ya wanamichezo Tanzania (SHIMIWI) ilifanyika Mkoani hivyo anaamini itaongeza ufanisi zaidi Tanga . katika ufanyaji kazi.

Ametoa pongezi hizo mara baada ya kupokea . vikombe viwili kutoka kwa wanamichezo walioshiriki kwenye michezo mbalimbali ikiwemo kuvuta kamba wanawake na wanaume, draft, mpira wa miguu,

“Licha michezo ikiwa ni ajira kwa wengine wanaoenda kwenye mashindano makubwa lakini kubwa ni kujenga afya mahusiano na kurelax kwakuwa huwezi kila siku uko ofisini tu unafanya kazi muda wote kwahivyo ni vizuri kuongeza ushiriki na wakati mwingine tutaweka ulazima wa watu kushiriki ili tuibue vipaji vingine vilivyojificha.” alisema Waziri Aidha Waziri Simbachawene amewataka viongozi wa Michezo wa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha wanaanzisha jogging club kwaajili ya kuendeleza michezo ili washiriki wanapokwenda SHIMIWI waweze kurudi na vikombe vingi zaidi.



Wadau wa Maendeleo wahimizwa kuchangia vifaa vya misaada ya kibinadamu wakati wa Maafa.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Alisema uungwaji mkono wa serikali Bunge na Uratibu Mhe. Umyy Nderiananga kutoka kwa wadau unasadia wananchi amewahimiza wadau wa maendeleo na watu kufikiwa na huduma kwa haraka binafsi kuendelea kushirikiana na Serikali kwa kutokana na majanga yaliyojitokeza kuchangia vifaa vya misaada ya kibinadamu ambayo husabababisha madhara kama wakati wa maafa. vifo, ulemavu wa kudumu, mali

Mhe. Umyy aliyasema hayo alipofanya ziara kuharibika pamoja na miundombinu. ya kikazi ya kutembelea na kukagua ghala la kuhifadhi vifaa vya misaada ya kibinadamu wakati wa maafa Kanda ya Kaskazini lililopo maeneo ya Chekereni, Wilaya ya Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro

“Nitoe wito kwa wadau na watu mbalimbali ambao wanaguswa kushirikiana na serikali kwa kutoa vifaa wafanye hivyo pengine ngaji ya Wilaya, Mkoa na hata kijiji ili tuwe navyo vya kutosha ili yanapotokea tunatoa msaada kwa haraka,” alihimiza Mhe. Ummu. Pia Mhe. Ummu alisisitiza utunzwaji wa magahala hayo hatua itakayosaidia vifaa hivyo kudumu kwa muda mrefu na kuwa tayari kutumika pindi vinapohitajika katika maeneo yenye maafa. Aidha aliupongeza uongozi wa mkoa wa Kilimanjaro kwa utayari wa kutoa msaada wa kibinadamu kwa wananchi wanaokumbwa na maafa kwa lengo la kuwasaidia kurejea katika hali yao ya awali. Kwa upande wake Mwakilishi wa Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Kilimanjaro ambaye ni Afisa Mifugo katika Mkoa huo Bwa. James Shao alisema ghala la Kanda ya Kasikazini linahudumia Mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga.



Watendaji waaswa kutunza vitendea kazi vya Ofisi

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Bwn. Kaspar Mmuya ametoa rai kwa watendaji wa serikali kutunza vizuri vyombo vya usafiri walivyopewa ili viweze kuwasaidia katika utendaji wa kazi na kudumu kwa muda mrefu.

Wito huo umetolewa wakati wa kukabidhi bajaji mbili kwa watumishi wa Ofisi ya Mpiga Chapa wa serikali jijini Dar es saalam katika kuwajengea Mazingira mazuri watu wenye ulemavu ya utendaji wa kazi.

“Ofisi ya Waziri Mkuu moja ya jukumu lake ni kuwezesha watu wenye ulemavu kwa kusimamia Sera ya Watu wenye Ulemavu na Miongozo ya watu wenye Ulemavu”

Akitoa neno la shukrani Bwn. Ophin Malley ameshukuru serikali kwa kuwatambua watu wenye ulemavu katika mazingira waliyonayo mahala pa kazi.

Jarida hili la Mtandao limeandaliwa
na kutolewa na
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na
Uratibu



KATIBU MKUU
Ofisi ya Waziri Mkuu
2 Mtaa wa Relini, S. L.P 980
40480 Dodoma,

Barua pepe; ps@pmo.go.tz, Simu; +255262322480
Fax: +255262324534, Tovuti: www.pmo.go.tz

